**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

**SHULE YA SEKONDARI MOSONGO,**

**S.L.P 43,**

**MUGUMU-SERENGETI.**

**10/ 12/ 2020.**

**Simu: +255(0) 787-183681**

**+255(0) 767-183681**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ……………………………………………………..**

**Ndg;**

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA KWANZA, SHULE YA SEKONDARI MOSONGO, MWAKA 2021

### 1. UTANGULIZI

Napenda kukujulisha kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga KIDATO **CHA KWANZA** katika shule yetu ya **MOSONGO SEKONDARI** iliyopo Kata ya Mosongo katika kijiji cha Mosongo kwa mwaka huu wa masomo **2021, HONGERA SANA**. Shule itafunguliwa mnamo **tarehe 11. 01. 2021** siku ya jumatatu. Mwanao anatakiwa kufika shulen tayari kwa kuanza masomo.

***Lugha ya mawasiliano shuleni ni kingereza tu.***

'KARIBU SANA'

…………………….

MARWA K. MAGIGE

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MOSONGO
MUGUMU - SERENGETI

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. SARE ZA SHULE

i. Sketi mbili (02) rangi ya **Ugoro,** (Kitambaa kizito, Namba moja) zenye marinda ya kawaida kumi na mawili(12) zinazovuka magoti (chini ya goti inchi 6) kwa wasichana.

*ii.* Suruali mbili (02) Rnngi ya **Ugoro,** (Kitambaa kizito, Namba moja), ***zisiszobana mwili*** zenye marinda na mifuko mwili ya kawaida mbele na mumoja nyuma, ziwe na mkunjo chini (Turn up). Kwa wavulana tu. ***Nimarufuku suruali aina ya modo kuvaliwa hapa shuleni.***

iii. Shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mifupi, ziwe na mfuko mumoja tu upande wa kushoto. Kwa wavulana na wasichana.

iv. T-shirt moja rangi ya kijivu, yenye kola.

v. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufungwa kwa kamba vyenye visigino vifupi na sio buti.

vi. Soksi jozi mbili nyeusi nzito zisiszo na alama/ mistari yoyote kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana.

vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kufungia suruali, kwa wavulana.

viii. Sweta rangi ya **Ugoro** isisyokuwa na alama nyingine yeyote. Iwe na shingo nyenye umbo la 'V'

ix. Rangi ya hijabu (kijuba) iwe nyeupe isiwe na urembo wowote, kw wasichana wa dini ya kiisilamu.

x. Raba za michezo, Bukta nyekundu kwa ajili ya michcezo.

**MUHIMU:**

***Nimeambatanisha kipande cha kitambaa cha suruali/sketi kinachotakiwa. Kama utapata shida kutambua rangi ya sare zilizotajwa hapo juu, tafadhali wasiliana na uongozi wa shule kupitia namba zilizo hapo juu kwa maelekezo zaidi.***

### B. MAHITAJI MENGINE MUHIMU NA YA LAZIMA KUJA NAYO SHULENI

i. KITI NA MEZA, vyenye fremu za chuma na top za mbao, kw ajili ya mwanafunzi kukalia darasani. Fuatilia maelekezo ya namna kinanyo takiwa kutengenezwa shuleni kulingana na mchoro ili kuepuka usumbufu.kumbuka hakuna viti shuleni, hivyo ni vema mwanao aje na kiti chake cha kukalia.

ii. Ream moja ya karataasi aina ya Double A kwa ajili ya matumizi shuleni.

iii. Fyekeo moja (01) kwa ajili ya kufanyia usafi shuleni

iv. Madaftari makubwa (counter Books) Quire 2, tisa (09) au zaidi.

v. Kalamu za kutosha

vi. Mkebe wa hisabati(mathematical set)/BOFA moja (01) lenye vifa vyake.

vii. Rula moja pamoja na kalamu za mkaa

viii. Faili moja kwa ajili ya kutunzia taarifa za maendeleo ya mwanafunzi shuleni.

ix. Kamsi ya kiingereza (English Dictionary)

x. Jembe moja (01) lenye mpini kwa ajili ya kufanyia usafi shuleni



MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MOSONGO
MUGUMU - SERENGETI

## C. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Sheria za shule ni kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Hivyo basi mwanafunzi anapaswa kuzifata bila kukiuka .ukiukwaji wa sheria za shule kama zilivyoonsesha hapa chini na zingine kwa mujibu wa sheria ya Elimu, utamfanya mwanafunzi aadhibiwe, asimamishwe masomo ama kufukuzwa shule kabisa.

**Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo muda wote awapo shuleni;**

i. Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wasio walimu, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na za nje ya shule kwa mujibu wa ratiba ya shule
iii. Kuwahi shuleni na kushiriki katika shughuli za shule na nyingine atakazopagiwa.
iv. Kuifahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu. A hakikishe anakuwepo ndani ya mipaka ya shule muda wote wa masomo anaotakiwa kuwa shuleni.
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vi. Kuvaa kwa unadhifu na uadilifu sare ya shule wakati wote awapo ndani na nje ya shule
vii. Kuzingatia na kutekereza ratiba ya shule ipasavyo
viii. Kutuza mali ya umma/ shule kwa umakini mkubwa.

**Makosa yafuatayo yatasababissha mwanafunzi kuadhibiwa:**

i. Kutokusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anaemzidi umri anapopita, au kuingia darasani au mahali pengine popote.
ii. Kutumia lugha zisizo na maadili mazuri dhidi ya mwalimuu, wanafunzi wenzake au mtu mwingie yeyote Yule.
iii. Kutovaa sare sahihi ya shule kwa unadhifu na uadilifu
iv. Kutkushiriki katika kazi zozote anazopewa na mwalimu ama viongozi wa serikali ya wanafunzi shuleni.
v. Kufuga ndevu(wavulana)
vi. Kutotii kengere ama kupuuza mwito wa kiongozi anaemuita
vii. Kutoheshimu picha za viongozi wa serikali (Raisi), Nembo ya taifa, Wimbo wa taifa, Bendera ya taifa na fedha za taifa.
viii. Kutokukubaliana na kuheshimu tofauti za kisisasa, kidini na kiutamaduni.
ix. Kutohudhuria vipindi darasani bila taarifa au ruhusa yeyote.
x. Kutohuduria kazi za mikono, mikuano ya shule, ukaguzi, makongamano, michezo, usafi wa mazingira n.k
xi. Kutokuwahi shuleni, na katika shughuli zozote alizopangiwa kulingana na ratiba ya shule.
xii. Kutokuwa nnadhifu kimavazi a usafi wa mwili kiujumula
xiii. Kutoiheshimu mipaka ya shule
xiv. Kuingia ofisi za walimu, maabara, jikoni, nyumba za walimu na wafanyakazi wengine wa shule bila ruhusa.
xv. Ni marufuku kkutembelea sehemu zifuatazo



MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MOSONGO
MUGUMU - SERENGETI

a) Vilabu vya pombe
b) Kumbi za starehe
c) Nyumba za wageni

xvi. Ni marufuku kucheza kamari ama michezo mingine inayofanana na hiyo, mfano Bonanza.

**Makosa yafuatayo akiyafanya mwanafunzi yatasababisha afukuzwe shule mara moja:**

i) Wizi
ii) Uasherati, ubakaji na ushoga
iii) Ulevi, uvutaji bangi na matumizi ya madawa ya kulevya ikiwemo sigara n.k
iv) Kupiga au kupigana shuleni
v) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule na umma kw aujumla
vi) Kudharau bendera ama wimbo wa taifa
vii) Kupata ama kusababisha mimba
viii) Kuoa ama kuolewa
ix) Kugoma,kuchochea ama kuongoza mgomo au kushiriki katika kuvuruga amani na usalama wa shule kwa namna yeyote ile
x) Kukataa adhabu kwa makusudi
xi) Kumiliki ama kutumia simu bila kibali/ ruhusa shuleni
xii) Kuwatesa ama kuwanyanyasa wanafunzi wenzake shuleni na hata nje ya shule.

**D. KUSAJILIWA:**

Mwanafunzi atasajiliwa siku ya kuripoti shule kama ilivyoelekezwa kwenye fomu hii hapo juu. Usajiri wote utafanyika ofisi ya mkuu wa shule. Mwanafunzi anatakiw akukabidhi fomu ya uthibitisho wa mwanafunzi na mzazi/ mlezi ikiwa imeambatanishwa na fomu ya uthibitisho wa Daktari (Medical examination form) kuhusu afya ya mwanfunzi zikiwa zimejazwa na kuthibitishwa na wahusika.

Kumbuka: fomu ya uthibitisho wa Daktari, lazima ijazwe na daktari baada ya kumpima mwanafunzi na kujua hali yake ya kiafya, kama maelekezo yalivyoelekeza kwenye fomu hiyo illiyoambatanishwa nyuma.

Vilevile fomu ya uthibitisho wa mwanafunzi na mazazi/ mlezi imeambatishwa nyuma ya fomu hii. Ijazwe na wahusik avizuri.kumbuka taarifa zinazojazwa zinatakiwa kuwa sahihi ili ziusaidie uongozi wa shule katika kumlea mwanafunzi.

Nakutakia maandalizi mema ya mwanao kujiunga na shule hii ya sekondari MOSONGO

**'KARIBU SANA'**

......................

**MARWA K. MAGIGE**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MOSONGO
MUGUMU - SERENGETI

## SHULE YA SEKONDARI MOSONGO

## FOMU YA UTHIBITOSHO/AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina la mwanfuzi ............................................ kidato ..................... Mwaka ..........

Shule ya msingi niliyosoma ..........................................liyoko kata ya ............................

SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/ WALEZI: -

i. Jina la Baba ....................................... anaishi kijiji .................. kata................
   Kazi yake .......................................... anwani yake .................. simu ..............
ii. Jina la mama ........................... ........Anaishi kijiji .................. Kata. ..............
   Kazi yake .......................... ... ........anwani yake ................... simu ............
iii. Jina la ndugu ........................... .......... anaishi kijiji.................... kata..............
   Kazi yake ........................................ Anwani yake ....................simu ..........

SEHEMU C: TAMKO LA MWANAFUNZI MWENYEWE

Mimi .................................................. Nakiri kuwa, nimezisoma vema na kuzielewa ipasavyo sheria, kanuni na taratibu za shule na kwamba naahidi: -

Kuzifuata sheria, kanuni na taratibu za shule kama zinavyoelekeza na natambua bila shaka yoyote kuwa sheria, kanuni na taratibu zote za shule zimewekwa kwa lengo la kunisaidia mimi kinidhamu na kitaaluma pia.

Kwenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule zinavyosema ni kosa na nitakuwa tayari kwa hatua stahiki za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu kwa lengo la kunirekebisha.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MOSONGO
MUGUMU - SERENGETI

**SHULE YA SEKONDARI MOSONGO,**

**S.L.P 43, MUGUMU-SERENGETI.**

## SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To the medical officer

…………………………..

…………………………

Name of the student……………………………………...From …………… Year ……………

Dear Doctor,

May you please examine the above mentioned student to confirm his/her fitness to undertaking Further studies

1. Urine …………………………………… 4. Stool ……………………………………..
2. Physical fitness………………………... 5. VD ……………………………………..
3. Tuberculosis ……………………………

## A. PRELIMINARY INFORMATION (By the student before the doctor)

| NO | DISEASE | YES/NO. | NO. | DISEASE | YES/NO. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pheumonia | | 11 | Ear, nose and trout | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operation (s) | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |

**B. MEDICAL EXAMINATION REPORT AND DOCTOR'S COMMENTS**

a) Weight
b) Heart beat
c) Vision

**C. MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider tha he/she is fit/unfit to undergo further Studies.

DOCTOR'S NAME AND SIGNATURE

…………………………………………………………………………………………...............

DATE AND OFFICIAL STAMP ……………………………………………………………………